MAISHA YANGU, CHAGUO LANGU.

Na Mwandishi, Lazaro Paschal Saranga.

DIBAJI

Hadithi ya *Maisha Yangu Chaguo Langu* ni kazi ya mwisho kati ya machapisho matano yaliyoandaliwa na Lazaro Paschal Saranga chini ya programu ya TFMB iliyoandaliwa na shirika la Readership for Learning(Soma) chini ya mradi wa Kestoria Kavazi. Machapisho haya yanajumuisha simulizi fupi na makala zinazochambua masuala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, na tamaduni zinazogusa maisha ya watu.

Katika orodha ya machapisho haya, tunapata simulizi fupi kama *Mbegu za Usawa* na *Mainda: Mti wa Ustahimilivu na Faraja*, ambazo zinatoa hadithi za maisha zilizojaa changamoto, matumaini, na mafanikio yanayohusiana na usawa na ustahimilivu. Makala kama *Faida za Usawa wa Kijinsia kwa Wanaume: Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa* inasisitiza umuhimu wa usawa wa kijinsia katika kuleta maendeleo ya jamii kwa ujumla, ikionyesha jinsi wanaume wanavyonufaika na mabadiliko haya. Aidha, makala *Upofu wa Jamii: Uhalisia wa Utamaduni wa Ubakaji Nchini Tanzania* inachambua kwa kina changamoto za kijamii zinazotokana na tamaduni potofu na athari zake kwa jamii.

Kazi hizi za mwandishi zinatoa mwanga wa kipekee kuhusu masuala ya kijamii yanayoikumba Tanzania, zikihamasisha mabadiliko chanya na kuleta uelewa mpana wa umuhimu wa usawa, ustahimilivu, na haki za binadamu. *Hadithi ya Maisha Yangu Chaguo Langu* ni mfano mzuri wa simulizi inayochangia katika ujenzi wa jamii yenye maarifa, huruma, na mshikamano.

~

Katika kijiji kidogo cha Nyabange, mkoani Mara, aliishi binti mmoja mrembo na mwenye maadili, aitwaye Bhoke mwenye umri wa miaka kumi na nane. Bhoke alikuwa binti wa pekee katika familia ya Mzee Magati na mkewe Mwani, wazazi wake walimpenda sana na kumjali binti yao wa pekee walijitahidi kumlea katika malezi mazuri, elimu bora na walimtimizia mahitaji yake yote kwa wakati. Bhoke alisoma shule ya awali mpaka sekondari mkoani Mara, Baba yake alimpenda sana na alitamani mwanaye asiende kusoma shule za mbali ili aendelee kumlea kwa ukaribu na kufatilia maendeleo yake siku kwa siku. Bhoke alibarikiwa uzuri wa muonekano na haiba, akili nyingi, na kipaji cha kufundisha na uongozi. Wakati kufundisha kwa watu wengine ni ujuzi wanaoupata kwa kufundishwa kwa Bhoke ilikua ni uwezo wa asili, alikua na uwezo mkubwa wa kuwafundisha watu wa aina zote hasa watoto na wakamuelewa na kupenda kufundishwa naye. Akiwa mwanafunzi alikuwa kiranja mkuu, shule ya msingi hata akiwa sekondari.Alikuwa na ndoto ya kuwa mwalimu na kumiliki shule yake binafsi ambayo ingetoa nafasi za kusoma kwa watoto wengi zaidi mkoani Mara na ajira kwa za ualimu na zinginezo kwa vijana na wanawake. “Mama mimi kabla ya kutimiza miaka arobaini nataka niwe ninamiliki shule ya msingi kwa watoto wakiume na wakike, kutwa na bweni. Pia nitatengeneza utaratibu wa kuwasaidia watoto ambao wanatoka katika familia zisizo na uwezo kupata nafasi ya kujiunga, wewe tuombe uhai tu” Bhoke alimwambia mama yake.

Mzee Magati na mkewe Mwani walijishughulisha na kilimo na ufugaji, waliishi maisha ya wastani yaliyowatosha kujikimu katika mahitaji yao yote ya msingi. Mzee Chota alikuwa rafiki wa karibu zaidi wa Mzee Magati, waliofahamiana miaka mingi tangu wakiwa watoto wadogo. Urafiki wao na familia zao umeendelea kwa muda mrefu hali iyosababisha hata watoto wao kuwa karibu pia. Mzee Chota alijulikana kijijini Nyabange kwa utajiri wa mali nyingi, mashamba, mifugo, mitumbwi ya ziwani na daladala zake zilizofahamika sana. Mzee Chota ana watoto wawili wa kiume ambao ni Hosea na Chanja. Hosea alikuwa na umri wa miaka ishirini na saba, alikuwa akifanya kazi ya kusimamia biashara za baba yake.

~

Baada ya kuhitimu kidato cha nne Bhoke na Hosea walianzisha mahusiano ya kimapenzi. Bhoke alipata mimba ya Hosea kabla ya matokeo ya mtihani wa taifa kutangazwa, Mzee Magati tofauti na hofu aliyokuwa nayo Bhoke hakukasirishwa sana baada ya kugundua aliyempa mimba ni kijana wa Mzee Chota kwasababu ya utajiri wa mali za baba yake na urafiki wao uliodumu kwa miaka mingi lakini Mwani alikasirika na kuumizwa sana na jambo lile alilia na alisikitika kwa uchungu “Magati binti yetu amepata mimba wakati bado ana safari ya masomo na ndoto zake kubwa za kuzitimiza, kwa mila na desturi zetu sasa ameshakuwa mke wa yule Kijana. Mimi ninashangaa jinsi hauna wasiwasi na umekubali matokeo kirahisi sana huoni kwamba tunakatisha ndoto za binti yetu mapema mno? Mwani alimhoji mume wake. Magati alimjibu Mwani “Hakuna tulichopoteza Mwani, binti yetu yuko katika familia salama, hatapata shida ataishi maisha mazuri hatafanya kazi za nguvu kama kilimo na

ufugaji kwasababu mme wake anasimamia mali ya baba yake atamlea kwa raha, na isitoshe yeye ni mwanamke tu hana ulazima wa kusoma sana mimi sioni kama kuna hasara yoyote”

Miezi mitatu baadaye matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha nne yalitangazwa na Bhoke aliifaulu kiwango cha daraja la kwanza, akipata alama A katika masomo yake yote. Wazazi wa pande zote mbili waliketi na kujadili hatima yake, na wakaamua kwamba Bhoke atakwenda kuishi na Hosea. Kwani kwa mila zao tayari hawa ni mke na mume. Japokuwa Mwani na Bhoke hawakufurahia uamuzi huu hawakuwa na budi bali kukubali kwasababu uamuzi wa Mzee Magati ni amri. Na Mzee Magati alikuwa na uhakika mwanaye ataishi maisha mazuri akiamini Hosea angekuwa kijana muungwana na muwajibikaji kama baba yake Mzee Chota.

Bhoke alienda kuishi na Hosea kama mke na mume, Mzee Chota alimpatia mzee Magati Ng’ombe watatu na shamba moja kama fidia na akampatia Hosea nyumba ya kuishi na Bhoke na kumwambia “Hosea umekua mwanaume sasa, jitegemee. Mlee mke wako na mtoto wenu atakayezaliwa kwa amani na upendo. Umeshakuwa mwanaume kamili fanya kazi tunza pesa ulipe mahari kwa Baba yake Bhoke na uandae harusi tuwaite ndugu wote waje kushuhudia ndoa yako. Usikawie fanya hima sisi tumeshazeeka tunahitaji kuibariki ndoa yako tukiwa hai”

Hosea alimshukuru baba yake, akamchukua Bhoke na kuhamia kijiji jirani ambako walianza maisha yao pamoja. Baada ya kujifungua Bhoke alikuwa mama wa nyumbani, alifanya kazi na kupika na usafi wa nyumba na Hosea alikwenda kazini kila siku kusimamia biashara zake na kumpatia taarifa baba yake.

~

Baada ya miaka miwili, Mambo yalianza kubadilika katika maisha yao. Hosea aliongeza mwanamke mwingine na kuzaa naye mtoto, alizidisha unywaji wa pombe na kurudi nyumbani usiku sana akiwa amelewa. Bhoke alilalamika sana kuhusu tabia ile lakini Hosea hakusikia. Bhoke alimwambia Hosea kwamba alitaka kurudi shule kuendelea na masomo “Hosea mtoto wetu ameacha kunyonya sasa nataka kurudi shule nikasome stashahada ya ualimu, mimi bado nina umri mdogo na nina vigezo vyote nina ndoto nyingi nnazo tamani kuzitimiza nimechoka kukaa nyumbani tu wakati nina mipango na maisha yangu inayohitaji kutimizwa”

Hosea alikasirishwa sana suala hili, aliwaza kwamba huyu mwanamke angemsumbua sana kama angemuoa kwani ameshaanza kutaka mambo makubwa yasiyo na ulazima kwa mwanamke, na kama angelimuoa angeleta ushindani na asingeweza kumtii. Hosea alikuwa na elimu ya kidato cha nne na mbali ya kuajiriwa na baba yake hakuwa na malengo makubwa zaidi ya hayo hivyo ndoto za maisha alizokuwa nazo Bhoke zilimtisha na kumnyima amani alihofia huyu Bhoke angemsumbua hapo baadaye na angemuacha endapo angemzidi kwa elimu na pesa.

Siku moja Hosea alirudi nyumbani usiku akiwa amelewa na alimwambia Bhoke “Mwanaume mwenye akili hawezi kusomesha mwanamke, nikusomeshe ili uniache ukaolewe na wanaume wengine? Kwani hapa kwangu unakosa kitu gani? Unavaa unakula vizuri na haufanyi kazi. Sasahivi tu haujakwenda tayari umeanza jeuri sasa mimi sitakuoa na sikuruhusu kwenda kusoma na hakuna mwanaume atakaye kuoa hapa kijijini kila mtu anajua wewe ni wa kwangu huwezi kuchukuliwa na mwanaume hadi mimi nikuache na mimi sikuachilii”

Bhoke alidhoofu na nuru yake ikafifia lakini ndoto zake bado zilikua hai. Bhoke alimwambia mama yake kwamba anatamani kuachana na Hosea na kuendelea na maisha yake peke yake, ajiendeleze na

masomo kwani bado ana umri mdogo na mmoja tu hawezi kumzuia kurudi shule na akamlea bila matatizo. Mama yake alimjibu “Bhoke mwanangu ninakuonea huruma na bado ninayo imani kubwa juu yako na ndoto zako, unanikumbusha mimi nikiwa msichana nilitaka nikasome ukarani lakini babu yako alinilazimisha kuorewa kwako sitakubari historia ijirudie, Baba yako anakupenda sana alikubali kukuozesha kwasababu alidhani utakua na amani kuolewa na kijana anayetoka familia yenye pesa rakini tukiongea naye akaerewa tabu unazopitia anaweza kubadiri mawazo yake”

Baada ya Mzee Magati kuongea na Mkewe, alipata uchungu alisikitika maisha anayoishi Bhoke hivyo alimuita nyumbani na kuzungumza naye Bhoke alimwambia baba yake kwamba bado anatamani kurudi masomoni na hana furaha kuishi na Hosea ni mateso na adhabu asiyostahili.

~

Baada kuona Maisha yanazidi kuwa magumu kwa Bhoke, wazazi wake walimrudisha nyumbani na kuishi naye. Magati hakuongea mengi lakini ndani ya moyo wake alijua maamuzi yake yalikuwa makosa makubwa na uonevu kwa binti yake aliyempenda sana, siku moja usiku alimwambia mke wake “Mama Bhoke nafikiri pengine nilifanya makosa kumuoza Bhoke kwa Chota, niliamini yule kijana angekua mtu makini kama baba yake lakini si hivyo. Sasa ninadhani tumuulize Bhoke anataka nini kama bado anataka kurudi shule tumpeleke Mwanza akasome”

Kwa furaha kubwa Mama Bhoke aliongea naye na Bhoke alisema yuko tayari kurudi shuleni na kumalizia masomo yake, wazazi wake wakafanya mpango wa kutafuta kituo cha elimu cha watahiniwa wa kujitegemea katika jiji la Mwanza. Bhoke alimuacha mtoto wake nyumbani na wazazi wake walimlea, akaenda kuendelea na masomo ya kidato cha tano na sita akiwa anaishi kwa Shangazi yake, siku za likizo alirudi kijijini kwao Nyabange kuwasalimu wazazi na kumuona mwanaye. Wazazi wa Bhoke walipata maoni na ushauri mbalimbali kutoka kwa wanakijiji wengine waliwapongeza kwa uamuzi wa busara na kishujaa wakikomboa maisha ya mtoto wao mapema na wengine waliwasema na kuwakosoa kwa kuvunja mila na desturi za jamii,” Yaani Mura umempokonya mkwerima wako mke, ati kisa nini? Erimu? Erimu gani kwa mwanamuke au unataka umuoe binti yako bhana? Harafu umevunja maadiri yetu Mura, kwasababu yure sasa japo urimzaa wewe ni mke wa mtu hawezi kufanya maamuzi yake bila ruhusa ya mume wake. Hawezi kuorewa, kurudi kwao wara kwenda kusoma mpaka mume wake amuachirie kabsa kabsa sasa unadhani ataorewa na nani pare kijijini na kira mtu anajua ni mwanamuke wa Hosea?” Mzee Marwa alimwambia Magati walipokutana kilabuni, Magati alimjibu kwa sauti ya chini “Marwa, kupitia hiri jambo nimejifunza somo kubwa, nirimkosea sana binti yangu kwa kumuoza kwa razima bira ridhaa yake kwa kijana wa Chota nikidhani atamtunza na kumpa maisha bora kumbe ni muhuni tu nimefanya maamuzi ya busara kumchukua na kumrudisha shureni akapambanie ndoto zake na najua atafanikisha kwani ana akiri na kipawa kikubwa cha uarimu”.

Marwa akamuuliza tena Chota “Sasa si akishamariza hiyo shure atarudimo hapa kijijini na ataorewa tena na Hosea ama utafanyaje?” Mzee Magati alijibu “Sasahivi sitamchaguria mume wa kumuoa na sidhani kama atakubari kurudi tena kwa yure kijana, na kwasababu hakua amemuoa hayuko chini yake

na binti yake hataperekeshwa na mira na desturi za ovyo ataorewa na mume wa chaguo rake.”

~

Baada ya kuhitimu kidato cha sita, Bhoke alijiunga na chuo kikuu cha Mtakatifu Augustino mkoani Mwanza ambako alisoma shahada ya kwanza ya ualimu. Wakati akiendelea na masomo yake ya chuo kikuu, alikutana na kijana aitwaye Tom, ambaye alimpenda kwa dhati. Uhusiano wao ulianza kama urafiki wa kawaida, lakini hatimaye ukakua na kuwa wa kimapenzi. Bhoke alimuadithia Tom historia ya maisha yake na mambo yote aliyoyapitia kijijini kwao, Tom alimuonea huruma Bhoke na kumuahidi atakua bega kwa bega kuhakikisha anamsaidia kutimiza ndoto zake. Tom hakujali kwamba Bhoke alizaa na mwanaume mwingine hapo awali, yeye alimpenda Bhoke jinsi alivyo na alitamani kuishi maisha yake na mwanamke mwenye ujasiri na upeo mkubwa kama Bhoke, Tom pia alikuwa na ndoto kubwa za kutimiza ili abadilishe maisha yake na ya mpenzi wake Bhoke.

Walipohitimu chuo kikuu, maisha yalianza kubadilika. Bhoke na mpenzi wake Tom wote walipata ajira. Bhoke aliajiriwa katika shule binafsi maarufu jinini mwanza, walimu na wanafunzi walimpenda sana Bhoke kwa ufundishaji wake. Ufaulu wa wanafunzi katika masomo aliyofundisha Bhoke uliongezeka. Tom alipata kazi serikalini na kwa pamoja wakaanza kushirikiana kutimiza ndoto za maisha yao. Tom alikuwa tofauti sana na Hosea, Tom alikua mpole na msikivu, alimjali na kumheshimu Bhoke pamoja na kazi yake. Na mara zote Tom alimshauri Bhoke kuongeza elimu na kujiboresha kitaaluma, walisaidiana katika kila jambo. Bhoke aligundua sasa Tom ndiye mwanaume wa chaguo lake, kwani alimpenda sio kwa huruma bali kwa upendo na heshima.

~

Baada ya mwaka mmoja tangu Bhoke na Tom wapate ajira. Tom alikwenda kijijini Nyabange kwa wazazi wa Bhoke kutoa mahari. Majirani na wanakijiji kwa ujumla walitarajia kuona Magati na Mkewe wakikakataa mahari ya Tom badala yake, Familia ya Magati walimpokea Tom na ndugu zake kwa bashasha kuu, waliwachinjia na mbuzi na kuwaalika ndugu na rafiki zao wakaribu kushiriki katika tukio hilo la kutoa mahari. Majirani walishangaa kuona Magati na mkewe wanavyopuuza mila na desturi kandamizi na kufanya maamuzi yao kulingana na maslahi ya Binti yao. Wazazi na ndugu wa Tom walimpenda sana Bhoke na walimkaribisha katika ukoo wao kwa heshima na upendo. Bhoke na Tom walifunga ndoa yao jijini Mwanza na Mzee Chota alihudhuria tafrija ile na alitoa zawadi ya ng’ombe wawili kwa Bhoke. Alimpongeza rafiki yake Mzee Magati kwa uamuzi wa busara wa kumnusuru Bhoke katika mahusiano mabaya. Hawakuwa na uhasama wala ugomvi kati yao urafiki na undugu baina yao uliendelea kama kawaida.

Wakati huu Hosea Chota alikuwa amezaa na wanawake watatu jumla ya watoto saba bila ya kufunga ndoa.

Ujumbe wa Mwandishi:

“Haki ya mwanamke kuchagua maisha yake haipaswi kufungwa na mila zinazomkandamiza”

MASWALI

1. Je unadhani ni kwanini Hosea alihofia Bhoke angemsumbua endapo angeenda kusoma na kutimiza ndoto za maisha yake?

2. Jamii ina mtazamo gani kuhusu mwanaume kumsomesha mpenzi wake?

3. Katika jamii yako kuna wanaume walio tayari kuwaunga mkono wake zao kujiendeleza kimasomo ili wafikie ndoto za maisha yao kama Tom?

4. Elezea mtazamo wa jamii yako kuhusu kuoa mwanawake aliyezaa na mwanaume mwingine?

5. Elezea jinsi Jina la hadithi linavyosadifu yaliyomo.?